## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MACHI, 2023 NA MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2023.

**Dondoo za tathmini ya Machi, 2023 na mwelekeo wa Aprili, 2023:**


Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Machi, 2023 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Aprili, 2023 nchini.

- Katika kipindi cha wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi 2023, upungufu wa mvua ulijitokeza katika maeneo mengi nchini kutokana na uwepo wa kimbunga *Freddy* na kisha kufuatiwa na ongezeko la mvua katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.
- Katika mwezi Aprili 2023, vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi sambamba na ongezeko la mvua katika baadhi ya maeneo.
- Hali ya joto ya kawaida inatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2023.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2023, maeneo mengi ya nchi yalitawaliwa na hali ya ukavu hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi kutokana na kutokea wa kimbunga Freddy. Hata hivyo, vipindi vya mvua vilijitokeza kwa baadhi ya maeneo katika wiki ya tatu na ya nne hivyo kuashiria kuanza kwa mvua za Masika katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, kuimarika kwa Ukandamvua na uwepo wa Wimbianga (*Madden-Julian Oscillation, MJO)* kulisababisha vipindi vya mvua kubwa vilivyopelekea mafuriko katika baadhi ya maeneo. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 117.8 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa kilichopo bandari ya Dar es Salaam (Dar Port) mnamo tarehe 19 Machi, 2023 ikifuatiwa na milimita 106.7 na milimita 90.2 vilivyopimwa katika kituo cha hali ya hewa cha

Arusha na kile kilichopo Ilonga, Morogoro mnamo tarehe 22 na 28 Machi, 2023 mtawalia. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi kwa siku ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1 hapo chini;




Kielelezo 1: Viwango vya mvua milimita 50 au zaidi vilivyopimwa kwa mwezi Machi, 2023.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2023

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani katika kipindi cha mwezi Aprili, 2023. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo kubwa la bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Aidha, katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola, hali ya joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani

inatarajiwa. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi Aprili 2023, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuimarika kidogo na hivyo kusababisha Ukandamvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2023

Kwa ujumla vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi. Hata hivyo, mvua za Msimu zinazoendelea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka zinatarajiwa kuisha kwa baadhi ya maeneo kuelekea mwishoni mwa mwezi. Kwa upande mwingine, hali ya joto ya kawaida inatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2023. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, upungufu wa mvua unatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, upungufu wa mvua unatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa kuendelea kwa baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Aprili, 2023. Aidha, upungufu kidogo wa mvua unatarajiwa kujitokeza wiki ya tatu ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, upungufu wa mvua unatarajiwa wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2023.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea kwa baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Aprili, 2023. Upungufu wa mvua unatarajiwa wiki ya tatu ya mwezi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Aprili, 2023. Aidha, upungufu kiasi wa mvua unatarajiwa wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2023.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Aprili, 2023. Upungufu wa mvua unatarajiwa kuelekea mwishoni mwa mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Aprili, 2023. Aidha, upungufu wa mvua unatarajiwa kuelekea mwishoni mwa mwezi.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**2.3 MATARAJIO KWA MWEZI APRILI, 2023.**

Katika kipindi cha mwezi Mei 2023, mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini hususan yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Kwa upande mwingine, ongezeko kidogo la hali ya joto inatarajiwa kujitokeza kwa maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua.

**2.4 USHAURI**

Mvua za msimu zinaendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza ikiwemo mafuriko.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Aprili, 2023 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz